

# احْـذَرْ
# إِنَّهُ دِيْنُ الشِّـيْعَـةِ

# TAHADHARI
# HIYO NDIO DINI YA SHIA (ITHNAASHARIA)


Tarjama:
Abdullaah Ghalib

Mwandishi:
Sheikh Rami Issa


www.islamic-invitation.com

# HAKIKA HIYO NDIYO DINI YA SHIA ITHNA-ASHARIA (RAAFIDHWA)

**Kila sifa njema anastahiki Allaah, Mwenye kuinusuru Sunnah na Uislamu, na Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake, Maswahaba wake na Mwenye kuwafuata hao mpaka siku ya malipo.**

**Ama baada ya hayo:**

**Hakika miongoni mwa mambo ambayo nyoyo huhuzunika, na macho hutiririsha machozi ni kuona kwamba waislamu wengi wamehadaiwa na pote la Shia Ithna-Asharia, mpaka wamedhani baadhi yao kwamba tafauti iliyopo baina yetu sisi (Sunni) na Shia (Ithna-Asharia) ni tafauti ya mambo ya Fiqhi tu, kama vile tafauti iliyopo baina ya Madhehebu nne zilizo mashuhuri (HANAFIYYAH, MAALIKIYYAH, SHAAFI'YYAH NA HANBALIYYAH).**

**Kutokana na ukubwa wa jambo hili nimekusudia kutaja baadhi ya ukweli ambao umefichikana kwa Waislamu walio wengi.**

# Ewe Ndugu yangu Muislamu:

## 1) Je unafahamu kuwa Shia Ithna-Asharia wanasema wazi kwamba hawamuabudu Allaah Mtukufu?!!!

**Anasema Rais wa Maulamaa wa Shia (Niimatullaahi Al-Jazaa-iriy): [Hakika sisi hatuungani pamoja nao -Ahlus Sunna- juu ya kumuamini Allah Muabudiwa, wala Nabii, wala Imam/khalifa, kwa sababu wao (sunni) wanasema: “Mola wao ni yule ambaye Mtume wake ni Muhammad, na khalifa wake baada yake ni Abu-bakri, na sisi hatumkubali Mola huyo, wala Nabii huyo, kwa sababu Mola ambaye Khalifa wa Nabii wake ni Abubakri sisi si Mola wetu, wala Nabii huyo si Nabii wetu ].**
**Huu ni ubainifu wawazi kuwa mashia hawamuabudu Allah mtukufu, bali wanamuabudu Allah ambae mtume wake sio Mu-hamad (Swala na Salamu Zimshukie)**




## 2) Je unafahamu kwamba miongoni mwa misingi ya Shia Ithna-Asharia ni kuitakidi kwamba Qur'an imepotoshwa?!!!

**Anasema sheikh wao Al-Mufid akinukuu maafikiano yao juu ya kupotoshwa kwa Qur'an: [wameafikiana Shia Imaamiyya juu ya uwajibu wa kurejea kwa (Ali Allaah amridhie), na pia wameafikiana juu ya kwamba Makhalifa waovu wamekhalifu mambo mengi katika kuitunga Qur'an, na wakapotosha ndani yake muqtadha wa kilichoteremshwa na Sunnah za Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) . Na (wanadai kwamba aliyemuita jina hili (la Al Mufid) ni Mahdi Imam wao wa 12, na akamwambia): "Ewe ndugu uliye mwema na rafiki mwongofu"].**

**Mpaka sheikh wao Nour At-Twabarsi (wanaemuita kiongozi wa Maimamu wa hadithi) amefikia kutunga kitabu alichokiita [Faslul khitwaab fii tahriif kitaabi Rabbil Arbaab], ametaja ndani yake riwaya Elfu mbili miongoni mwa riwaya zao zenye kutegemewa zinazo thibitisha kuwa Qur'an hii tulionayo si sahihi.**

**Na wale waliojitokeza kulipinga hilo katika miaka ya karibuni katika maimamu wa kishia ni kwa sababu ya Taqiyya tu wa kuchelea siri yao isifichuke mbele ya waislam wote.**


سورة الولاية
بسم الله الرحمن الرحيم
يا ايها الذين امنوا بالنبي والولي الذين بعثناهما
ليهديانكم الى صراط مستقيم نبي وولي بعضهما
من بعض وانه عليم خبير ان الذين يوفون بعهد الله
لهم جنات النعيم والذين اذا تليت عليهم اياتنا كانوا

## 3) Je unajua kuwa Maulamaa wa Shia Ithna-Asharia wanadai kwamba Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) aliwahi kunyonya katika matiti ya Ami yake Abu Twalib?!!!

**Amepokea sheikh wa Mashia Muhammad Bin Yaqoub Al-Kulain "wanamuita Thiqatul islaam" katika kitabu chake (Al-Kaafi) ambacho ni kitabu tegemezi kwao, amesema: imepokewa kutoka kwa Abu Baswiir kutoka kwa Abu Abdillaah (Alayhis salaam) amesema: [Wakati alipozaliwa Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) alikaa baadhi ya masiku bila ya kupata maziwa, Abu Twalib akamuweka katika matiti yake na Allaah akateremsha ndani yake maziwa, akanyonya baadhi ya masiku mpaka Abu Twalib alipompata (mjakazi) Halima As-Sa'diyya akampatia ].**



## 4) Je unajua kuwa Maulamaa wa Shia Raafidhwa wanawatuhumu Malaika kwamba wao wanamuasi Allaah na wanamchukia Ali Bin Abi Twalib?!!!

**Amepokea Sheikh wao Abu Jaafar As-Swaffaar "wanamuita At- thiqatul Jaliil wal-Muhaddithil Nnabiil" kutoka kwa Abu Abdillaahi (alayhi Ssalaam) amesema: [Allaah aliutangaza Ukhalifa wa Amiirul Muuminiin "Ali" Malaika wakakubali isipokuwa Malaika mmoja anaeitwa Futwrus na Allaah akalivunja bawa lake ].**

**Na hali ya kuwa Allaah anasema:**

**[Hawamuasi Allaah kwa alilowaamrisha na wanafanya walio amrishwa ].**



**5) Je unajua kwamba Maulamaa wa Shia Raafidhwa wanadai kuwa Iblis alikuwa anampenda Ally (Allaah amridhie) na anamtetea?!!!**

**Amepokea Sheikh wao As-Swaduuq "Wanamuita Imamu wa zama zake" kutoka kwa Imam Ally amesema: [Nilimfuata Iblis mpaka nikamfikia, nikamvamia na kumuangusha chini, nikamkalia kifuani kwake na nikamkaba shingo yake ili nimnyonge, akasema: (Usifanye hivyo ewe Abul Hasan, hakika mimi ni mwenye kupewa muhula (muda) mpaka siku ya wakati maalum , Wallaahi ewe Ally, hakika mimi nakupenda sana, na hakuna yeyote anayekuchukia wewe ila yule ambaye nimeshirikiana na baba yake katika kumuingilia mama yake na akawa ni mtoto wa zinaa). (amesema Ally: [nikacheka na nikamuachilia!! ].**



**6) Je unajua kwamba Maulamaa wa Shia Ithnaasharia wanadai kuwa mtu yeyote hawezi kuwa Shia mpaka awalaani Maswahaba na wakeze Mtume (Swala na Salamu Zimshukie)?!!!**

**Amesema Sheikh wao Muhammad Baaqir Al-Majlis "wanamuita Hoja na Fakhari ya Umma": [Itikadi yetu katika kujitenga: sisi tunajitenga na Masanamu manne, Abubakri, Umar, Uthmaan na Muawiya, na tunajitenga na wanawake wanne, Aisha, Hafsa, Hindu na Ummul Hakam, na wote wenye kuwafuata hao, na kwamba hao ni viumbe wa Allaah walio na shari Zaidi juu ya ardhi, na hakika haitimii Imani mbele ya Allaah na Mtume wake na Maimamu (12) isipokuwa baada ya kujitenga na maadui zake ].Na pia akadai kwamba: [Abubakri na Umar ndio Fir'aun na Hamaan wa Umma huu ].**



**7) Je unajua kwamba Maulamaa wa Shia Ithna-Asharia wanamtuhumu Abubakri (Allaah amridhie) kwa kusema kwamba alikuwa anaswali nyuma ya Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) hali ya kuwa amevaa sanamu shingoni mwake akilisujudia?!**

**Amesema Rais wa Maulamaa wao anayeitwa Niimatullaahi Al Jazaairiy: [Usishangae kwa hadithi hii: hakika imepokewa katika hadithi (za Maimamu 12) kwamba Abubakri alikuwa anaswali nyuma ya Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) na hali kuwa kuna sanamu (ametundika) katika shingo yake analisujudia ].**



## 8) Je unajua kwamba Maulamaa wa Shia Ithnaashasharia wanadai kuwa Umar (Allaah amridhie) yuko motoni anaadhibiwa kwa adhabu kubwa Zaidi ya Iblis (shetani)?!

**Amesema Rais wa Maulamaa wao Niimatullaahi Al Jazaairiy: [Imepokewa katika hadithi za Maimamu (12) kwamba shetani atafungwa kwa minyororo sabini ya chuma kutoka motoni na atakokotwa kuletwa katika uwanja wa hesabu, ataangalia atamuona mtu mbele yake anaongozwa na Malaika wa adhabu hali ya kuwa katika shingo yake amefungwa minyororo ya motoni mia moja na ishirini, shetani atamkaribia na atasema: (Amefanya nini muovu huyu mpaka amenizidi mimi katika adhabu na hali ya kuwa mimi nimewapoteza viumbe na nimewaingiza katika maangamivu?). Atasema Umar kumjibu shetani: (Sijafanya jambo lolote kubwa isipokuwa mimi nimepora Ukhalifa wa Ally Bin Abi Twalib ].**



**9) Je unajua kwamba Maulamaa wa Shia Ithna-Asharia wanamtuhumu Uthman Bin Affaan (Allaah amridhie) mkwe wa Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) kuwa alikuwa mnafiki tena kafiri?!**


**Amesema sheikh wao Niimatullaahi Al Jazaairiy: [Alikuwa Uthmaan katika zama za Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) ni miongoni mwa wale walio dhihirisha Uislamu wao na kuficha ukafiri ]. Bali wanawalazimisha wafuasi wao kumchukia Uthmaan Bin Affaan (Allaah amridhie) kumkufurisha na kuvunja heshima yake, mpaka amefikia kusema sheikh wao Al Karkiy: [Hakika yule ambaye katika moyo wake hamchukii Uthmaan, havunji heshima yake wala haitakidi ukafiri wake mtu huyo ni adui wa Allaah na Mtume wake, amekufuru yale aliyo teremsha Allaah ].**



**10)Je unajuwa kwamba Ally Bin Abi Twalib (Allaah amridhie) pia hakusalimika na matusi ya Shia Ith-na-Asharia?**
**Amesema Ally Bin Ibrahim Al-Qummi (miongoni mwa Maulamaa wao wakubwa wenye kutegemewa) kuhusu tafsiri ya aya:**

**(Hakika Allaah haoni haya kutoa mfano hata wa mbu au ulio zaidi yake ).**

**Amesema: [Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillaahi (alaihi salaam) kwamba Allaah amepiga mfano huu kwa Amirul Muuminiin (alaihi salaam), kwa sababu makusudio ya Mbu hapo ni (Ally) Amirul Muuminiin (alaihi salaam), na aliye zaidi yake ni Mtume (Swala na Salamu Zimfikie) ]. Kisha Mujtaba Sshiiraz akaongeza kwa kusema: [Hii ni riwaya tukufu kwamba imamu wetu ni Mbu!!].**






**11) Hivi unafahamu kuwa Maulamaa wa Shia Ithna-Asharia wanamtuhumu mama wa waumini Aisha (Allaah amridhie) kwa dhambi ya uzinifu ambayo Allaah amemtakasa nayo?!!**

**Amesema Al-Qummi na Al-Majlis kuhusu tafsiri ya aya inayosema:**

**[Allaah amewapigia mfano walio kufuru (ambaye ni) mke wa Nuh na Lut, walikuwa chini ya waja wetu wema wawili lakini wakawafanyia khiyana ].**

**Amesema: khiyana hapo maana yake ni zinaa, na Aisha atapigwa haddi (Adhabu ya uzinifu) kwa kile alichofanya akiwa njiani kutoka Basra ].**

**-Maana yake ni kwamba Mahdi wao wa uwongo atakuja na kumfufua Aisha (Allaah amridhie) kutoka kwenye kaburi lake kisha atampiga haddi ya uzininifu.**
**-Na pia ametaja sheikh wao Rajab Al-Bursi ambaye wanamuita Al-Haafidh kwamba Aisha (Allaah amridhie) alikusanya Dinari arobaini za uzinifu na kuzigawa kwa watu wanaomchukia Ali (Allaah amridhie ).**
**Wamethubutu kumuitwa Mama Aisha Allah amridhie kuwa ni muovu kama walivyo sema katika chanel ya (Fadak) na chanel zinginezo.**
**Je, Unaridhia matusi haya kwa mama yako mama Aisha kipenzi cha Mtume Amani zimshukie????**



**12)Hivi unafahamu kuwa Shia Raafidhwa wanaitakidi kwamba Abubakri, Umar, Aisha na Hafsa (Allaah awaridhie) wameshirikiana kumuuwa Mtume (swala na salamu zimfikie)?!!**

**Ametaja sheikh wao Al-'Ayyaash ambaye wanamuita (Al-Muhaddithul Jaliil) katika tafsiri yake, kutoka kwa Abu Abdillaah amesema: [Hivi mnadhani Mtume amekufa au ameuwawa?], Allaah anasema: (Hivi akifa au akiuwawa ndiyo mtarudi nyuma kwa visigino vyenu?), Aisha na Hafsa walimnywesha sumu kabla ya mauti yake, tukasema: hakika wao na baba zao (Abubakri na Umar) ni viumbe wa shari mno ].**

**- Kisha Majlis akasema kwa kutilia nguvu maneno ya Al-'Ayyaash: [Hakika 'Ayyaash amepokea riwaya kwa sanadi yenye kuzingatiwa kutoka kwa Jafar Swaadiq kamba Aisha na Hafsa wakishirikiana na baba zao wamemuuwa Mtume (swala na salamu zimfikie) kwa kumnywesha sumu ].**



## 13) Hivi unafahamu kuwa Shia Ithna-Asharia wanawatuhumu Masunni kwamba ni watoto wa zinaa?!!

**Amepokea sheikh wao Al-Kulain (wanamuita Thiqatul islaam) riwaya inayosema: [watu wote ni watoto wa zinaa isipokuwa Shia wetu ].**




## 14) Hivi unajua kuwa Shia Ithna-Asharia wanadai kwamba kuzuru kaburi la Hussein (Alaihis salaam) siku ya Arafa ni bora kuliko Hija na Umra mara milioni moja?!!

**Amepokea sheikh wao Hurrul Aaamiliy (wanamuita Al-adiibul Faqiih wal-Muhaddithul kaamil) riwaya kwamba Jafar Swaadiq amesema:[Mwenye kuzuru kaburi la Hussein siku ya Arafa Allaah anamuandikia (malipo ya) Hija milioni moja ambazo amehiji pamoja na Mahdi, na (malipo ya) Umra milioni moja akiwa pamoja na Mtume (swala na salamu zimfikie), na (malipo ya) kuacha huru watu Elfu moja na Farasi Elfu moja waliobeba shehena (ya mizigo) kwa ajili ya kupigana jihadi katika njia ya Allah (kwa ajili ya Allaah). Na Allaah atasema: Mja wangu Aliye mkweli, ameamini ahadi yangu, na Malaika watasema: Fulani ni mkweli Allaah amemtakasa kutoka juu ya Arshi yake ].**
**Na hizi ni mbinu na jitihada za kutaka kuwafanya mahujaji wasiende arafa badala yake walielekee kaburi la Husein lililopo Karbalaa.**



## Hivi unajua kwamba Shia Ithna-Asharia wanaitakidi kwamba Mahujaji wote ni Yonda (Nyani) na Nguruwe isipokuwa Shia tu?!!

**Amesema sheikh wao Abu Jafar Swaffaar ambaye (wanamuita At-thiqatul Jaliil wal-Muhaddithul Nnabiil) kwamba amepokea riwaya kutoka kwa Abu Baswir amesema:[Nilihiji pamoja na Abu Abdillaahi, zamani tulipokuwa kwenye twawafu nilimuuliza, hivi Allaah atawasamehe watu hawa? Akasema: "Ewe Abu Baswir, hakika watu wengi unaowaona hapa ni Yonda/Nyani na Nguruwe" nikamwambia nionyeshe, amesema: akazungumza baadhi ya maneno kisha akapangusa usoni wangu kwa mkono wake nikawaona wao kuwa ni Yonda na Nguruwe, likaniogopesha hilo, kisha akanipangusa tena nikawaona kama walivyokuwa mwanzo ].**



## Tanbih:

**1) Hakika kwa maneno yaliyo tangulia inakurubia Milima kuanguka kutokana na ubaya wake "Laa haula wala Quwwata illa billaah".**

**2) Vitabu hivyo vilivyo tajwa hapo juu ni vitabu vya kutegemewa mbele ya Shia na watunzi wake ni watu bora kwao na pia huwasifia kwa sifa mbalimbali kutokana na juhudi yao katika kutumikia Ushia.**

**Swali:**
**Je watu wenye itikadi hizi ni Waislamu?!**



Autor : **Rami Isa**

+201111012626

RAMY_EASA2016

RAMYESSA2018

www.islamic-invitation.com